# BWANA ALITUTENDEA MAMBO MAKUU

***Alex Rwelamira***
***25.11.2024***
***DSM***




1. Bwana alipowarejeza mateka wa Sayuni, tulikuwa kama waotao ndoto/
   Ndipo kinywa chetu kilipojaa kicheko/
   Na ulimi wetu kelele za furaha.
2. Ndipo waliposema katika mataifa, Bwana amewatendea mambo makuu/
   Bwana alitutendea mambo makuu/
   Tulikuwa tukifurahi.
3. Ee Bwana, uwarejeze watu wetu waliofungwa, kama vijito vya kusini/
   Wapandao kwa machozi/
   Watavuna kwa kelele za furaha.
4. Ingawa mtu anakwenda zake akilia, azichukuapo mbegu za kupanda/
   Hakika atarudi kwa kelele za furaha/
   Aichukuapo miganda yake.